Tanzania Public Health Association
(*Chama cha Afya ya Jamii Tanzania*)

WITO KWA WANANCHI WOTE KUCHUKUA TAHADHARI DHIDI YA UGONJWA UNAOSABABISHWA NA VIRUSI VYA KORONA 2019

Chama cha Afya ya Jamii Tanzania (*Tanzania Public Health Association*, TPHA) ni chama kinachoundwa na wataalamu wa Afya ya Jamii chenye madhumuni ya kuunga mkono juhudi za Serikali, wananchi na wadau mbalimbali katika kuendeleza Afya ya Jamii hapa nchini. Moja ya jukumu lake ni kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali ya Afya ya Jamii kwa kutumia ushahidi wa kisayansi.

Ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Korona 2019 (COVID-19) ulianza kuenea duniani kutokea Wuhan, nchini China mwezi Desemba 2019. Machi 2020 ugonjwa huu uliingia Tanzania. Serikali ilichukua hatua za haraka katika kupambana na janga hili, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kikosi kazi cha Korona katika ngazi mbalimbali, chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Pamoja na majukumu mengine, kikosi kazi kilikuwa na jukumu la kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji wa maambukizi kwa watu wanaoingia nchini kupitia viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu. Hususani, kuimarisha uwezo wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii na kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujikinga na ugonjwa huo ambao hauna tiba, na wakati huo hakukuwa na chanjo.

Njia kuu zilizohamasishwa ni kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na kuepuka misongamano. Aidha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaasa Watanzania kumtanguliza Mungu, ambapo aliitisha siku tatu za maombi maalumu. Pia, ili kuondoa wasiwasi na hofu iliyokuwa imetanda nchi nzima, Serikali iliamua kutoweka katazo la kutotoka nyumbani au kusafiri "lockdown" kwa kuwa ingekuwa na athari zaidi kuliko faida. Kwa sehemu kubwa wananchi kila mahali walihamasika na kutekeleza maelekezo kama inavyotakiwa. Vile vile, kutokana na juhudi za wataalam na watafiti wa hapa nchini, tiba asilia ikiwemo matumizi ya dawa za mitishamba na mchanganyiko wa virutubisho vya asili vinavyotumika kwa kunywa au kufukiza mvuke (*kupiga nyungu*) zimegundulika na kutumika kwa wagonjwa.

TPHA inatambua kuanzia Desemba 2020 kuwepo kwa taarifa kutoka mahospitalini, makanisani, misikitini na jamii kwa ujumla, kuhusu ongezeko la vifo vitokanavyo na maradhi yanayoathiri mfumo wa upumuaji, unaoambatana na dalili za kukohoa, homa, mafua, mwili kukosa nguvu hususani katika kundi la watu wenye umri mkubwa. Dalili hizo zimekuwa zikihusishwa na COVID-19, hasa kutokana na **lahaja** (variant) mpya ya virusi vya Korona iliyogundulika Afrika Kusini na nchi nyingine duniani. Kasi ya kusambaa na madhara ya COVID-19 yanayosababishwa na **lahaja** mpya ya virusi vya Korona yamethibitishwa kuwa ni makubwa. Kutokana na mabadiliko hayo, Serikali imetahadharisha wananchi kuchukua hatua za kujikinga na

kuhakikisha wagonjwa wenye dalili za magonjwa yanayoathiri mfumo wa upumuaji waweze kupata huduma stahiki.

Kamati kuu ya Chama cha Afya ya Jamii Tanzania, **inatambua** juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali na wadau mbalimbali katika kupambana na janga la COVID-19 nchini kwetu. Hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha janga hili haliathiri sana uchumi na maisha ya watu kwa ujumla. **Tunatambua** kuwa hadi sasa, pamoja na utafiti, tiba ya COVID-19 haijapatikana. Hata hivyo afua mbalimbali zimependekezwa na kuchukuliwa kupunguza madhara ya janga hili ikiwa ni pamoja na mbinu zinazopunguza madhara yake kwa wagonjwa kama vile kujifukiza (*kupiga nyungu*), kutumia lishe bora, matumizi ya oksijeni na dawa za kupunguza athari za virusi hivyo mwilini mwa mgonjwa.

TPHA inatambua vyema nguvu ya tahadhari za kuchukua dhidi ya magonjwa yanayoathiri mfumo wa kupumua – ikiwa ni pamoja na kuepuka misongamano isiyo ya lazima, usafi binafsi ikiwa ni pamoja na uvaaji wa barakoa, na matumizi ya vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizi kwa watoa huduma (*Personal Protective Equipment*). Tunatambua pia nguvu ya majadiliano na uwazi katika uanishaji wa mbinu (afua) bora za kujikinga dhidi ya milipuko ya aina hii.

TPHA aidha inatambua kuwa kwa sasa chanjo dhidi ya Korona zimegunduliwa na makampuni mbalimbali duniani. Baadhi ya chanjo hizo zimeruhusiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kutumika kwa dharura kwa makundi yaliyo kwenye umri hatarishi na maeneo ya kazi hatarishi. Aidha, gharama za chanjo hiyo ni kubwa. Ingawa Shirika la Afya Duniani limetangaza msaada kwa nchi zisizo na uwezo, kiasi kinachotolewa kwa kila nchi ni kidogo na hakiwezi kukidhi idadi ya watu wote nchini. Ili chanjo iwe na manufaa, inatakiwa itolewe kwa asilimia 60 hadi 80 ya wananchi ili kupata kinga kwa wote. Hivyo, basi ni vyema kila mmoja wetu akaendelea kuzingatia mbinu/afua zilizoanishwa kujikinga na maambukizi ya Korona.

TPHA inaunga mkono uamuzi wa Serikali kutoweka katazo la watu kutoka majumbani kwao na kusafiri nje ya makazi yao kwa kuwa itaathiri wananchi wengi wanaotegemea kipato cha kila siku na itaathiri pia shughuli za uzalishaji na upatikanaji wa huduma za jamii ambayo itadumaza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, TPHA inatoa mapendekezo yafuatayo:

1. **Kuvaa Barakoa na kunawa Mikono kwa Maji Tiririka**

Wananchi wote wachukue tahadhari dhidi ya magonjwa yanayoathiri mfumo wa kupumua katika kipindi hiki cha maambukizi yaliyojitokeza baada ya wimbi la awali ambapo nchi yetu iliweza kulikabili janga hilo kwa kiasi kikubwa. Hivyo, kila mtu kuanzia viongozi wavae barakoa kwenye vyombo vya usafiri, viwanja vya mipira, shuleni/vyuo, sokoni, nyumba za ibada, na pale ambapo inabidi kushiriki kwenye matukio/maeneo yenye misongamano.

TPHA inatoa wito kwa viongozi wa ngazi zote za Serikali kuwa mfano wa kuigwa katika kuzingatia tahadhari hizi za kujikinga dhidi ya COVID19 na magonjwa mengine na kuzitekeleza kwa vitendo.

2. **Uthibiti wa Ubora wa Barakoa**

Asasi za kiraia, mashirika ya dini, na taasisi za umma zishiriki kutoa elimu (kwa wajasiriamali na kampuni za ndani) ya utengenezaji na ufungashaji wa barakoa za vitambaa zenye viwango bora. Elimu hii itasaidia watu wengi kutengeneza barakoa zenye viwango na kuuzwa kwa bei nafuu kwa wananchi walio wengi kama ilivyofanyika wakati wa wimbi la kwanza la mlipuko wa Korona.

TPHA inatoa wito kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zifanye ukaguzi na kuondoa sokoni barakoa zote zinazotiliwa shaka kuwa si salama kwa afya ya mtumiaji. Hii itatoa nafasi kwa Watanzania kuwa na uhakika wa barakoa zinazopatikana kwa matumizi baada ya kuthibitishwa na mamlaka zetu.

3. Utafiti na Uhakiki wa Chanjo

TPHA inatoa wito kwa watafiti nchini kuandaa maandiko na kutafuta fedha kutoka serikalini na vyanzo vingine ili kufanya utafiti wa chanjo ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti-tathmini wa chanjo zilizokwisha patikana na kuona kama zipo zinazofaa kutumika kwenye mazingira yetu. Ni vyema kama taifa tukawekeza katika kufanya utafiti ili kuainisha afua nyingine katika kupambana na ugonjwa huu.

4. Elimu kwa Umma

Magonjwa mengi yanayosababishwa na virusi vya Korona yana muingiliano kati ya wanyama na binadamu, TPHA inashauri Serikali kuendelea kuimarisha utekelezaji wa dhana ya *AFYA MOJA* inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni vyema basi, sekta mbalimbali zikashiriki katika kupambana na janga hili. Ushirikishwaji wa wadau uwe kwenye mfumo wa Kamati/Vikosi Kazi ili moto wa kuhimiza tahadhari na kinga uendelee na kushika kasi, na uwe wa kudumu.

5. Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Kinga na Tiba

Watanzania wote, mashirika, taasisi, kampuni, wawekezaji na marafiki wa Tanzania tuwe mstari wa mbele katika juhudi za kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa kinga, vifaa tiba na virutubisho vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya kwa wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali za umma na binafsi. Hili ni muhimu kupunguza gharama za kuhudumia wagonjwa, na kuwakinga wahudumu wa afya dhidi ya maambukizo kutoka kwa wagonjwa.

Mwisho, tunatoa wito kwa Matawi yote ya TPHA, wanachama wetu wote, vyombo vya habari, asasi za kiraia, mashirika ya dini na wadau wote kufanya kila liwezekanalo kuhimizia jamii kuchukua tahadhari katika kuzuia maambukizi na kuenea kwa mlipuko huu. Aidha TPHA, ikishirikiana na serikali na wadau wengine, itawajengea watendaji wa ngazi zote uwezo wa kudhibiti magonjwa ya mlipuko kwa kuzingatia dhana ya Afya Moja.

Imetolewa kwa maelekezo ya mkutano wa dharura wa Kamati Kuu ya Taifa uliofanyika tarehe 20/02/2021, kwa niaba ya Chama Cha Afya Jamii Tanzania.

Dr. Philbert Nyinondi
MWENYEKITI